Katika mstari wa kwanza, Paulo anaamuru ya kwamba dua, sala na maombezi yafanyike kwa ajili ya watu wote. Katika tafsiri ya lugha halisi ya Kigriki ambayo Paulo alitumia, neno alilotumia kwa wote ni “anthropos”, ambayo ni neno linalojumuisha wote waume kwa wake. Paulo anatumia neno lile lile tena katika mstari wa nne anaposema, Mungu. . .**“*anataka watu wote waokolewe na kufikia ujuzi wa kweli.*”** Lakini, mstari wa nane Paulo anapozungumzia kuongoza katika maombi, anatumia neno Mwanaume. Katika lugha ya Kigriki neno hilo ni “aner**.”** Neno hili linatumika pale tu inapomaanisha wanaume. Haijumuishi wanawake kamwe! Kwa hiyo amri ni kwa wanaume tu kuongoza katika maombi ya kanisa ya hadhara.

Kuna tofauti iliyowazi kati ya mstari wa nane unaosema ya kwamba wanaume wanaamuriwa kusalisha kila mahali na mstari wa kumi na moja ukiwaamuru wanawake kujifunza kwa utulivu, akitii kwa kila namna. Neno “kutii” inatoka kwenye neno la kigiriki la kijeshi likiwa na maana “kuwa chini ya.” Katika mstari wa kumi na mbili, Paulo anaandika: ***“Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha au kuwa na mamlaka juu ya mwanaume, bali awe katika utulivu.*** Alijua alichokua akifanya na alifanya dhambi ile na Hawa makusudi kabisa huku akijua ni dhambi.

Wanawake wana sehemu nzuri tu ya kumhudumia Mungu. Kuzaa watoto si laana iliyoletwa na anguko la pale Edeni, bali ni baraka toka kwa Mungu kwa wanawake katika uumbaji (Mwa 1:28; Mwa 3:16). Wanawake pia wanauwezo wa kuwa waalimu, si kwa wanaume, bali kwa wanawake wengine na watoto (2 Timotheo 1:5; Tito 2:3-5). Wanawake wakristo, kama vile Priscilla, wanaweza kusaidia waume zao katika ufundishaji wengine pembeni (Mdo 18:24-26). Mfano wa kimungu wanawake wakristo hufundisha wengine kwa tabia yao njema (1 Petro 3:1,2).

Amani hudumu katika kanisa na Mungu kufurahishwa pale ambapo wanaume na wanawake kwa pamoja wanamtumikia katika nyanja aliyowaumba.

Wanawake haiwapasi kuwa wazee, mashemasi, wahubiri au wanenaji wa hadhara katika ibaada ya Mungu. Lakini kazi yao ya kuwa wamama wazuri na waalimu wa watoto wao na wanawake wengine ni muhimu. Kwa moyo mnyoofu hebu tutii mapenzi ya Mungu!!!

Kwa maelezo zaidi, Tafadhali kuwa huru kuwasiliana nasi

KWA MAWASILIANO:
KANISA LA KRISTO.
P.O.BOX 150 BUNDA TZ, KANISA LA KRISTO 27 MASAKTA HANANG', KANISA LA KRISTO 210 KAKAMEGA KENYA

NAFASI YA MWANAMKE KATIKA KANISA.

Nafasi ya mwanamke katika jamii leo inajadiliwa kwa upana sana. Ushawishi wa vuguvugu la Ukombozi wa mwanamke "au" watetezi wa wanawake unatikisa ulimwengu. Watu wengu waume kwa wake wanakubaliana ya kwamba yatupasa kuwa na usawa katika ajira na malipo ya ajira hizo. Wengine pia wanakubaliana ya kwamba ni vizuri kuwa na haki sawa chini ya sheria kwa mwanamke kama ilivyo kwa wanaume. Hata hivyo, wakristo waume kwa wanawake ni lazima wakanushe baadhi ya madai haya ya vuguvugu ya kutetea wanawake kwani yako kinyume na matakwa ya Mungu.

Katika kanisa la Bwana leo, wapo wengi wanaouliza nafasi ambayo wanawake wanayo. Wengine wanadai ya kwamba wanawake wanahaki ya kuongoza mikutano ya injili, Kuhubiri,na hata kuhudumu kama wazee. Wamemezwa na vuguvugu la uetetezi wa wanawake au na madhehebu, haswa wapentekosti, ambao wanaruhusu wanawake kufanya kila kitu anachokifanya mwanaume katika kanisa.

Wakristo wanataka kufanya matakwa ya Mungu. Matakwa ya Mungu kuhusu nafasi ya mwanamke katika kanisa inafunuliwa katika kitabu chake, Biblia (2 Timotheo 3:16,17). Lazima tufuate Biblia kama twahitaji kumpendeza Mungu na kupata uzima wa milele.

Bibilia yasemaje?

Nafasi ya mwanamke katika kanisa ni ipi?

Kuna sehemu ambapo wanawake na wanaume wako sawa mbele ya Mungu. Upendo wa Mungu ni sawa kwa wote (Yohana 3:16). Mungu hana upendeleo kwa yeyote inapofikia swala la wokovu (Mdo 10:34,35). Wanaume na wanawake lazima watii mpango wa mungu wa wokovu na watapata baraka sawa (wagalatia 3:26-28).

Hata hivyo, vipo nyanja ambapo mpango wa Mungu unatofautiana na ule wa wanaume. Katika familia, Mungu amemteua mwanaume kuwa kichwa (Waefeso 5:23). Mwanaume yampasa kuhudumia famila yake kimwili na Kiroho (Mw 3:17-19; 1 Timotheo 5:8; Waefeso 6:4). Wanawake wana nafasi muhimu katika mpango wa Mungu ambayo wanaume hawana. Wanawake ni wasaidizi kwa waume zao, walimu wa watoto wao na watunzaji wa nyumba zao (Mw 3:16; Waefeso 5:22-24; Tito 2:4,5). Wanaume na wanawake ni tofauti kijinsia na kisaiklojia.

Eneo ambalo Mungu amemteua kila mmoja inamfaa kama Mungu alivyowaumba.

Kuna maandiko kadhaa inayohusiana na nafasi ya mwanamke katika kanisa. Katika 1 Wakorintho 11:3, Mtume Paulo aliandika: ***"Lakini nataka mfaamu ya kuwa kichwa cha kila mwanaume ni Kristo, kichwa cha mwanamke ni mwanaume, na kichwa cha Kristo ni Mungu."*** Mwanaume ana kichwa

ambacho lazima awajibika kwalo – Yesu Kristo. Mwanamke pia ana kichwa ambacho ni lazima awajibike kwalo-- mwanaume. Lakini hata Kristo pia ana kichwa anayowajibika kwalo – Mungu Baba. Kristo si zaidi ya Mungu kwasababu anawajibika kwake. Pia

mwanamke si zaidi ya mwanaume kwa kuwa anawajibika kwake. Nafasi aliyomteuwa mwanume na mwanamke haiusiani na uzaidi na ukubwa. Inahusiana na sababu ya Mungu kuwaumba.

Timotheo wa kwanza, sura ya pili, ni mstari muhimu sana inayohusiana na nafasi ya mwanamke katika kanisa. Paulo anazungumza kuhusu kuongea katika hadhara au katika mikutano ya ibaada ya nje (public speaking) wanapokutana pamoja (1 Timotheo 2:1,2; 1 Timotheo 3:14,15).